# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1030

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Elimu Jumuishi Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali, Msingi na Elimu Malumu

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-813-2

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Elimu Jumuishi Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali, Msingi na Elimu Malumu nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA ELIMU JUMUISHI STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA AWALI, MSINGI NA ELIMU MAALUMU

**2023**

©Taasisi ya Elimu Tanzania, 2023
Toleo la Kwanza, 2023

ISBN: 978-9987-09-813-2

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa Somo la Elimu Jumuishi Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali, Msingi na Elimu Maalumu.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo

Orodha ya Majedwali ........ iv
Vifupisho ........ v
Shukurani ........ vi

1.0 Utangulizi ........ 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania ........ 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu ........ 2
3.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu ........ 2
3.2 Malengo mahususi ya Elimu ya Ualimu ........ 2
4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ualimu ........ 3
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........ 3
6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 4
6.1 Mkufunzi ........ 4
6.2 Mwalimu tarajali ........ 4
6.3 Mzazi ........ 5
7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 5
8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 5
9.0 Upimaji ........ 6
10.0 Idadi ya Vipindi ........ 7
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 7
Bibliografia ........ 11

# Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi .......... 3

Jedwali Na. 2.1: Alama za Upimaji Endelevu .......... 7

Jedwali Na. 3 1: Maudhui ya somo .......... 8

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |

# Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa Somo la Elimu Jumuishi Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali, Msingi na Elimu Maalumu yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha uandaaji wa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala. Vilevile, TET inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya kusimamia kazi ya maboresho ya mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwaandaa wahitimu wenye maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndio lengo kuu la uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Elimu Jumuishi ni somo la jumla litakalosomwa na walimu tarajali wote wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali, Msingi na Elimu Maalumu. Somo hili lina lengo la kumwandaa mwalimu tarajali mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ujifunzaji ili kujenga maarifa, stadi na mwelekeo chanya kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu. Aidha, Somo la Elimu Jumuishi lina lengo la kumwandaa mwalimu tarajali mwenye umahiri wa kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji wa shule ya msingi, kwa kuzingatia misingi ya ujumuishi ili kuleta usawa, haki na elimu bila ukomo. Vile vile, mwalimu tarajali atajifunza namna ya kuchambua dhana nzima ya elimu jumuishi itakayomwezesha kuwatambua wanafunzi wenye mahitaji maalumu na kutoa afua stahiki. Pia, somo hili litamwezesha mwalimu tarajali kumudu mbinu za kutumia zana zinazozingatia ujumuishi.

Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kumuongoza mkufunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Elimu Jumuishi Tanzania Bara. Aidha, muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu wa Mwaka 2023. Maudhui ya muhtasari huu yamejikita katika Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea inayosisitiza utoaji wa elimu inayomwezesha Mtanzania kujitegemea na kumudu maisha yake ya kila siku.

Hivyo, muhtasari huu utamwezesha mkufunzi kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji kwa kumjengea mwalimu tarajali stadi za udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika mazingira yake. Aidha mwalimu tarajali atajifunza namna ya kuchopeka masuala mtambuka na kutumia TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu nchini Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;
(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;
(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;
(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu

### 3.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu

Kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

### 3.2 Malengo mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo mahususi ya Elimu ya Ualimu ni kumwandaa mwalimu kuwa mahiri katika:
(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu;
(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;
(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kukuza stadi za utambuzi wa awali kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;
(g) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji; na
(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani *classroom-based action research*).

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ualimu

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwalimu tarajali ni:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji;
(b) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(c) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri;
(d) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
(e) Kutumia, TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kumtambua mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;
(g) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji;
(h) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (*instructional leadership*); na
(i) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani *classroom-based action research*).

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Sehemu hii inawasilisha umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa na mwalimu tarajali kama ulivyoanishwa katika Jedwali Na 1.

**Jedwali Na. 1.1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi*

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumudu misingi ya elimu jumuishi | 1.1 Kuchambua dhana ya elimu jumushi<br>1.2 Kumudu mbinu za kumtambua mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu katika ujifunzaji<br>1.3 Kumudu mbinu za kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu katika ujifunzaji |
| 2.0 Kumudu misingi ya kuwezesha ujifunzaji wa kila mwanafunzi katika mazingira jumuishi | 2.1 Kumudu matumizi ya mbinu na zana zinazozingatia mahitaji ya ujifunzaji ya kila mwanafunzi |

## 6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji hutegemea ushirikiano na mahusiano mazuri baina ya mwalimu, mwanafunzi, mzazi/mlezi, jamii, na wadau wengine wa elimu. Mkufunzi anashauriwa kuwashirikisha wadau hao ili kufanikisha mchakato huo wa ujifunzaji. Muhtasari huu umebainisha majukumu yao kama ifuatavyo:

### 6.1 Mkufunzi

Mkufunzi anatarajiwa:

(a) Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21 kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji zitakazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji. Baadhi ya mbinu zinazopendekezwa ni zile zinazosaidia kukuza uwezo wa kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kufaragua zana;

(c) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwalimu tarajali bila kujali tofauti zao; na

(d) Kubaini mahitaji maalumu ya mwalimu tarajali na kumpatia afua stahiki.

### 6.2 Mwalimu tarajali

Mwalimu tarajali anatarajiwa:

(a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mafunzo ndani na nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa anajenga umahiri stahiki katika maeneo mbalimbali ikiwemo usimamizi wa ufundishaji na ujifunzaji, mbinu za kufundishia na mbinu za upimaji zitakazomwezesha kubaini mafanikio na kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika mafunzo endelevu kupitia shule zilizo jirani na chuo kwa lengo la kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo. Baadhi ya nadharia hizo ni haiba, maandalizi ya somo, kutumia mbinu za kufundishia, kuandaa na kutumia vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kutathmini wanafunzi;

(c) Kufanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na weledi katika fani ya ualimu;

(d) Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji; na

(e) Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.

### 6.3 Mzazi

Mzazi/mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji; na
(b) Kumpatia mwalimu tarajali mahitaji muhimu pamoja na vifaa vinavyotumika katika ujifunzaji.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Elimu Jumuishi utaongozwa na ujenzi wa umahiri unaotumia mbinu zinazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji na mkufunzi kuwa mwezeshaji. Mkufunzi atatumia mbinu zinazomshirikisha mwalimu tarajali katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji anuai na uwezo wa mwalimu tarajali. Mbinu hizo ni pamoja na zile zinazomwezesha mwalimu tarajali kuwa na fikra tunduizi, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali na kushiriki katika kutoa mrejesho. Njia nyingine ni ziara za kimasomo, kazi za vitendo, majadiliano katika vikundi, igizodhima, kazimradi, fikiri-andika-jozisha-shirikisha, utafiti, uwasilishaji, masimulizi, michezo mbalimbali na mbinu nyingine kulingana na muktadha ili kufanikisha ujifunzaji.

Mkufunzi anashauriwa kumwongoza mwalimu tarajali kuwa mbunifu na mnyumbufu katika kutumia mbinu shirikishi wakati wa mazoezi ya ufundishaji na kufaragua zana za ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia mazingira halisi ya mwanafunzi.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa kuwa shirikishi na zinazokidhi mahitaji ya ujifunzaji na uwezo wa mwalimu tarajali. Mkufunzi anapaswa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yake. Pia, anapaswa kufaragua zana ambazo zitamsaidia mwalimu tarajali kujenga tabia ya udadisi, ugunduzi na kukuza fikra tunduizi. Mkufunzi anapaswa kuhakikisha mwalimu tarajali anapata nafasi ya ama kuona, kusikia au kugusa zana bila kuhatarisha afya na hali ya mwalimu tarajali. Vilevile, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa zimsaidie mwalimu tarajali kuelewa kinachofundishwa na kutumia milango ya fahamu katika ujifunzaji. Baadhi ya zana za ujifunzaji na ufundishaji zilizopendekezwa ni pamoja na sidii zenye maudhui ya dhana ya elimu jumuishi, matini zinazohusu zana za ubainishaji wa mapema kwa mwanafunzi, picha na michoro mguso inayoonesha mazingira jumuishi, video zinazohusu utoaji wa afua stahiki na dodoso la ubainishaji. Baadhi ya zana zimependekezwa katika jedwali la maudhui katika safu ya zana.

## 9.0 Upimaji

Upimaji wa maendeleo ya ujifunzaji wa mwalimu tarajali utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji. Zana zinazotumika katika upimaji ni zile zitakazozingatia ujenzi wa umahiri kwa mwalimu tarajali. Mkufunzi anapaswa kuhakikisha anampima mwalimu tarajali katika nyanja zote za upimaji ambazo ni maarifa, stadi na mwelekeo. Aidha, ni muhimu kufanya tathmini ya maendeleo ya mwalimu tarajali ili kubaini kiwango cha utendaji alichofikia katika nyanja zote za ujifunzaji. Matokeo ya tathmini yatasaidia kufanya uboreshaji ili kuhakikisha malengo ya Elimu ya Ualimu Elimu Maalumu yamefikiwa.

Mkufunzi anapaswa kubuni shughuli nyingi zaidi za upimaji ili kuchochea ujifunzaji. Aidha, mwalimu tarajali atapimwa kwa upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utachangia asilimia sabini (70%) na upimaji tamati utachangia asilimia thelathini (30%). Mwalimu tarajali anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia hamsini (50%) na upimaji tamati kwa angalau kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafaulu, mwalimu tarajali anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu. Jedwali Na. 2 linaonesha mgawanyo wa alama katika upimaji endelevu.

**Jedwali Na. 2.1:** *Alama za Upimaji Endelevu*

| Na | Shughuli za upimaji | Mgawanyo (%) |
|---|---|---|
| 1 | Mtihani wa Mhula wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 2 | Mtihani wa Mwisho wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 3 | Mtihani wa Mhula wa Mwaka wa Pili | 6.0 |
| 4 | Kazi Mradi | 7.0 |
| 5 | Mkoba wa Kazi | 5.0 |
| | **Jumla** | **30** |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari huu unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 60. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi viwili (2) kwa wiki.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari huu umebeba maudhui ambayo yamepangiliwa katika vipengele sita (6) ambavyo ni: Umahiri mkuu, umahiri mahususi, vigezo vya upimaji, shughuli za ujifunzaji, zana na idadi ya vipindi. Jedwali Na. 3.1 linaonesha maudhui ya somo.

**Jedwali Na. 3.1:** *Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji*

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu misingi ya elimu jumuishi | 1.1 Kuchambua dhana ya elimu jumuishi | Kuchambua dhana na misingi ya elimu jumuishi | Dhana na misingi ya elimu jumuishi imechambuliwa. | Matini zinazohusu elimu jumuishi, picha, michoro na michoro mguso inayoonesha ujumuishi | 10 |
| | 1.2 Kumudu mbinu za kumtambua mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu katika ujifunzaji | (a) Kufafanua dhana ya ubainishaji wa mapema wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu katika ujifunzaji | Dhana ya ubainishaji wa mapema wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu imefafanuliwa | Matini zinazohusu dhana za ubainishaji, vifaa vya ubainishaji vinavyopatikana kwenye mazingira na dodoso la ubainishaji | 25 |
| | | (b) Kuchanganua viashiria vya mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kwa kuhusianisha na hatua za ukuaji | Viashiria vya mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu vimechanganuliwa | Matini zinazohusu viashiria vya mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu, video, picha, michoro, michoro mguso inayoonesha makundi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu na dodoso la ubainishaji | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuchambua mbinu na zana za ubainishaji wa mapema kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji | Mbinu na zana za ubainishaji wa mapema kwa mtoto mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji zimechambuliwa | Matini zinazohusu zana za ubainishaji wa mapema kwa mwanafunzi, vifaa vya ubainishaji vinavyopatikana kwenye mazingira na dodoso la ubainishaji | |
| | 1.3 Kumudu mbinu za kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu katika ujifunzaji | (a) Kufafanua dhana ya afua kulingana na mahitaji mbalimbali ya mwanafunzi | Dhana ya afua kulingana na mahitaji mbalimbali ya mwanafunzi imefafanuliwa | Vifaa saidizi, matini zinazohusu afua stahiki, dodoso la ubainishaji, picha, michoro mguso na video zinazohusu utoaji wa afua stahiki | 16 |
| | | (b) Kuhusianisha afua kulingana na mahitaji mbalimbali ya mwanafunzi | Afua kulingana na mahitaji mbalimbali ya mwanafunzi imehusianishwa | Vifaa saidizi, picha, michoro mguso na video zinazohusu utoaji wa afua stahiki | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kumudu misingi ya kuwezesha ujifunzaji wa kila mwanafunzi katika mazingira jumuishi | 2.1 Kumudu matumizi ya mbinu na zana zinazozingatia mahitaji ya ujifunzaji ya kila mwanafunzi | (a) Kuchambua mbinu na zana rafiki na fikivu za ujifunzaji katika mazingira jumuishi | Mbinu na zana rafiki na fikivu za ujifunzaji katika mazingira jumuishi zimechambuliwa | Matini zinazohusu ujumuishi, zana rafiki na fikivu zinazopatikana katika mazingira, picha na michoro mguso zinazoonesha mazingira jumuishi | 19 |
| | | (b) Kumudu mbinu za kuboresha mazingira ya malezi, ufundishaji na ujifunzaji katika elimu jumuishi | Mazingira ya malezi, ufundishaji na ujifunzaji katika elimu jumuishi yameboreshwa | Matini zinazohusu ujumuishi, picha, michoro mguso na video zinaonesha ujumuishi | |

## Bibliografia


Conroy, M.A. (2019). *Outcome of best in class on teacher's use of effective practice: Self-efficiency and classroom quality*: University of Florida.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2022). *Mwongozo wa utekelezaji wa mkakati wa taifa wa elimu jumuishi 2022-2026*: Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Machera R. (2017). Teaching intervention strategies that enhance learning in higher education. *Universal journal of education Research*, 5(5), 733-743. Doi: 10.13189/ujer 2017.050505.

Ministry of Education. (2018). *National pre-tertiary education curriculum framework*. Ghana Ministry of Education.

Ministry of Education Science and Technology. (2017). *National strategy for inclusive education 2018-2021*. Ministry of Education Science and Technology.

United States Agency for International Development [USAID]. (2020). *Mbinu za ujifunzaji kwa wote: Mbinu za ufundishaji kwa walimu wa skuli za msingi na madarasa ya awali kwa kuzingatia mfumo wa elimu mjumuisho*. Mwongozo wa Mwalimu. USAID.